

# Kupata Rekodi ya Chanjo ya COVID-19



Swahili

## Jinsi ya kupata rekodi ya chanjo yako ya COVID-19

Uthibitisho wa chanjo yako ya COVID-19 utarekodiwa kwenye **immunisation history statement** (taarifa ya historia ya kuchanjwa) baada ya kupata chanjo yako.

Mara umepokea dozi zote zinazohitajika, utaweza pia kupata **COVID-19 digital certificate** (cheti cha dijitali ya COVID-19) yako.

Unaweza kupata uthibitisho wa chanjo yako ya COVID-19 kupitia:

- **Medicare online account** (akaunti ya mtandaoni ya Medicare)
- **Express Plus Medicare app** (programu ya Medicare ya Haraka Ziada)
- **My Health Record** (Rekodi Yangu ya Afya)
- **Individual Healthcare Identifiers Service** (Huduma ya Vitambulisho vya Afya Binafsi)
- **Australian Immunisation Register** (Rejesta ya Chanjo ya Australia)



### Akaunti ya mtandaoni ya Medicare

1. Ingia akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na chagua **Medicare**
2. Kutoka sehemu ya **Immunisation history** (historia ya chanjo), chagua **View immunisation history** (Tazama historia ya chanjo)
3. Chagua jina lako
4. Bonyeza kwa **View immunisation history statement (PDF)** (Tazama taarifa ya historia ya chanjo) au **View COVID-19 digital certificate (PDF)** (Tazama cheti cha dijitali ya COVID-19)

### Programu ya Medicare ya Haraka Ziada

1. Fungua programu na ingia
2. Kutoka sehemu ya **Services** (Huduma), chagua **Immunisation history** (Historia ya chanjo)
3. Chagua jina lako
4. Bonyeza kwenye **View immunisation history statement (PDF)** (Tazama taarifa ya historia ya chanjo) au **View COVID-19 digital certificate (PDF)** (Tazama cheti cha dijitali ya COVID-19)

### Rekodi Yangu ya Afya

Unaweza pia kupata uthibitisho wa chanjo zako za COVID-19 kutoka Rekodi Yangu ya Afya.

Ikiwa tayari una Rekodi Yangu ya Afya:

1. Ingia kwenye akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na chagua **My Health Record (Rekodi Yangu ya Afya)**
2. Fungua Rekodi Yangu ya Afya
3. Pata thibitisho ya chanjo zako kutoka ukurasa wako wa **Record Home** (Rekodi Nyumbani) au kutoka ukurasa wako wa **Immunisations view (Mtazamo wa chanjo)** chagua **Documents** (Nyaraka), **Immunisations**

Ikiwa huna Rekodi Yangu ya Afya lakini una kadi ya Medicare:

1. Ingia kwenye akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na unganisha na **My Health Record** (Rekodi Yangu ya Afya)
2. Thibitisha utambulisho wako na unda Rekodi Yangu ya Afya, na hakikisha kuchagua 'Ndio' kuweka ndani habari ya chanjo (habari ya Medicare) katika Rekodi Yangu ya Afya yako
3. Fungua Rekodi Yangu ya Afya yako
4. Pata thibitisho ya chanjo zako kutoka ukurasa wako wa **Record Home** (Rekodi Nyumbani) au kutoka ukurasa wako wa Mtazamo wa Chanjo

# Kupata Rekodi ya Chanjo ya COVID-19

## Huduma ya Vitambulisho vya Afya Binafsi (ikiwa huna kadi ya Medicare)

Ikiwa huna kadi ya Medicare na unataka kupata thibitisho ya chanjo zako mtandaoni, utahitaji Kitambulisho cha Afya Binafsi (IHI). Ikiwa huna IHI, unaweza kuomba kimoja mtandaoni.

Kwa maelezo zaidi ona:

[www.servicesaustralia.gov.au/individuals/services/medicare/individual-healthcare-identifiers/how-get-ihl](http://www.servicesaustralia.gov.au/individuals/services/medicare/individual-healthcare-identifiers/how-get-ihl)

Mara tu unayo IHI, unaweza kupata thibitisho ya chanjo zako kupitia myGov.

1. Ingia akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na chagua **Individual Healthcare Identifiers service** (huduma ya Vitambulisho vya Afya Binafsi)
2. Kutoka sehemu ya **Services** (Huduma), chagua **Immunisation History** (Historia ya Chanjo)
3. Bonyeza kwa **View immunisation history statement (PDF)** (Tazama taarifa ya historia ya chanjo) au **View COVID-19 digital certificate (PDF)** (Tazama cheti cha dijitali ya COVID-19)

## Rejesta ya Chanjo za Australia

Ikiwa huwezi kupata thibitisho ya chanjo zako za COVID-19, pigia simu kwenye

**Australian Immunisation Register (Rejesta ya Chanjo ya Australia)** kwa **1800 653 809** kati ya 8am-5pm (saa 2 asubuhi hadi saa 11 jioni), Jumatatu hadi Ijumaa.

Uwaombe watumie kwako **immunisation history statement** yako (taarifa yako historia ya chanjo).

Inaweza kuchukua hadi siku 14 kufika kwa njia ya posta.


Ikiwa unahitaji mkalimani, tafadhali pigia simu kwa **Translating and Interpreting Service (TIS) (Utafsiri na Ukalimani wa Simu)** kwa **131 450**.

## Viungo Muhimu

Kwa habari zaidi juu ya jinsi ya kupata taarifa yako ya historia ya chanjo **scan the QR code below** (tambaza nambari ya QR hapa chini)



Ili kujua zaidi juu ya Mpango wa Chanjo za COVID-19 katika NSW **scan the QR code below** (tambaza nambari ya QR hapa chini)



**Scan the QR code below** (tambaza nambari ya QR hapa chini) kupata njia ya rahisi sana mtandaoni kupata thibitisho ya chanjo zako za COVID-19.

